HABARI KUTOKA
KAMISHENI YA WAKFU
NA MALI YA AMANA
Muharram 16, 1448 AH
01/07/2026
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa huduma bora za Hijja, Zakka, Wakfu, Amana, Mirathi na Baytul-mal
0051

# TAARIFA YA KATIBU MTENDAJI WA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA KATIKA HAFLA YA UWASILISHAJI WA RIPOTI YA HIJJA MWAKA 1447H/2026M

## JULAI 1,2026 - NYUMBA YA SHERIA MAZIZINI



***Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi Kamisheni ya wakfu na Mali ya Amana Profesa Issa Haji Ziddy (Kulia) akimkabidhi Waziri wa (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Alhajj, Mhe. Haroun Ali Suleiman ripoti ya Hijja ya mwaka 1447 / 2026 Mazizini Zanzibar 01/07/2026***

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya RaisKatiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora,
Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana,
Viongozi wa Serikali, Dini na Taasisi za Hijja,
Waandishi wa Habari,
Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana.
Assalamu Alaikum Warahmatullahi Wabarakatuh.

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia afya na fursa ya kukutana katika hafla hii muhimu ya uwasilishaji na makabidhiano ya Ripoti ya Hijja kwa mwaka 1447H/2026M. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azikubali ibada za mahujaji wetu wote, awajalie salama na atupe tawfiki ya kuendelea kuhudumia wageni Wake kwa uadilifu, uaminifu na weledi wa hali ya juu.

Hijja ni miongoni mwa nguzo tano za Uislamu, na ni ibada inayohitaji maandalizi ya kina, usimamizi makini na utekelezaji unaozingatia masharti ya Sharia na ustawi wa mahujaji. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: “Na timizeni Hijja na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.” (Al-Baqarah: 196). Aya hii inatukumbusha kuwa Hijja s iibada ya kiroho pekee, bali pia ni amana ya kitaasisi inayohitaji kutekelezwa kwa uwajibikaji, uwazi na uadilifu na kwa kuzingatia haki za mahujaji, taasisi na kila mhusika.

Mheshimiwa Waziri, Kwa mujibu wa Sheria, Kamisheni ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Hijja Zanzibar. Leo, nimepata heshima ya kuwasilisha mukhtasari wa Ripoti kabla ya Mwenyekiti wa Kamisheni kukukabidhi rasmi Ripoti hiyo ya Hijja.




***Mwenyekiti wa " Peace Travel & Tours" Alahaj. Zulfikar Sadik Othman (Kulia) akimkabidhi zawadi Rais wa Afisi kuu ya Hijja Tanzania Alhaj Abdulla Talib abdulla wakati wa makabidhiano ya ripoti ya Hijja ya mwaka 1447 / 2026 Mazizini Zanzibar 01/07/2026***

Kwa miaka mingi, Kamisheni ilijikita katika jukumu la kuwezesha (facilitation) huduma za Hijja. Mfumo huo umechangia mafanikio makubwa katika sekta ya Hijja Zanzibar na Tanzania na kufungua mlango wa Mfuko wa Hijja na Ziara au utalii wa Kiislamu. Hata hivyo, mabadiliko ya kimfumo yanayoletwa na Serikali ya Saudi Arabia yameweka mazingira mapya yanayohitaji Kamisheni kuimarisha zaidi jukumu lake la uratibu na usimamizi hasa ukizingatia kuwa shughuli za Hijja kwa sasa ni kazi ya mwaka mzima.

Hivyo, Kamisheni inaingia katika hatua mpya ya kuhakikisha mfumo wa Hijja unakuwa wa kitaasisi zaidi, wenye uwazi wa gharama, viwango vinavyolingana vya huduma kwa kuzingatia daraja, na uwajibikaji wa pamoja kati ya wadau/wahusika wote. Hatua hii haikusudii kupunguza nafasi ya taasisi za Hijja, bali kuimarisha usawa, ushindani wa haki na ulinzi wa maslahi ya mahujaji, viongozi na wahusika wote.

Mheshimiwa Waziri, Katika kufanikisha hilo ,Kamisheni kwa kushiriana na Wizara imeandaa Muongozo Mpya wa Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Hijja, unaolenga :-

- Uwazi wa gharama,
- Viwango vya huduma,
- Mikataba ya wazi,
- Ukaguzi wa huduma,
- na mfumo wa kushughulikia malalamiko

Muongozo huu utaimarisha ushindani wa haki na kuongeza ubora wa huduma.

Mheshimiwa Waziri, Jumla ya mahujaji 4,000 pamoja na viongozi 40 wa Tanzania walitekeleza ibada ya Hijja mwaka huu ukilinganisha na 3600 wa mwaka jana. Wanawake walikuwa 2,070 (51.75%), na wanaume 1,930 (48.25%). Kwa upande wa usimamizi, mashirika ya Zanzibar yaliwahudumia 2,652 (66.3%), huku ya Tanzania Bara yakihudumia 1,348 (33.7%). Hii inaonesha mchango mkubwa wa taasisi za Zanzibar katika huduma za Hijja.

Mahujaji walikuwa na umri na marika tofauti kuanzia watoto, vijana na watu wazima. Zaidi ya 37.5% ya mahujaji walikuwa na umri wa miaka 60 na kuendelea, jambo linalosisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma mahsusi za afya, uangalizi wa wazee na maandalizi ya kitabibu kabla ya safari.

Uchambuzi wa hali ya kijamii na kiuchumi umeonesha kuwa Wastaafu walikuwa ni



***Waziri wa (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Alhajj, Mhe. Haroun Ali Suleiman (kati kati) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Kamisheni ya Wakfu na viongozi wa Taasisi za Hijja mara baada ya kupokea ripoti ya Hijja ya mwaka 1447 / 2026 Mazizini Zanzibar 01/07/2026***

29.1%, Wafanyabiashara 24%, Waajiriwa Serikali ni 19%, Sekta binafsi ni 16.5% na Makundi mengine ni 11.4%. Hali hii inaonesha mchango mkubwa wa ukuaji wa uchumi na mafao ya kustaafu katika kupatikanaji fursa ya Hijja kwa wananchi wetu.Aidha, kunaonesha umuhimu wa kuzingatia mapumziko maalumu kwa mahujaji hasa baada ya kurudi Hijja. Mheshimiwa Waziri.

Bado Tanzania tuna fursa ya kuhiji zaidi mara moja kwa mwenye uwezo. Hata hivyo, 70.9% ya mahujaji walikuwa wanahiji kwa mara ya kwanza, jambo linaloonesha kuwa walikuwa wageni katika mazingira ya Hijja na walihitaji uangalizi wa karibu.Kwa msingi huo, Kamisheni itahakikisha upatikanaji wa :-

- Mafunzo ya lazima kwa mahujaji wapya,
- Mtaala wa pamoja wa mafunzo ya Hijja,
- Kuimarisha matumizi ya teknolojia za kidijitali , na
- Kuimarisha uwezo wa walimu wa Hijja na viongozi wa misafara.

Mheshimiwa Waziri. Katika huduma za usafiri, safari tisa za moja kwa moja zilihudumia mahujaji 2,562 (64%), huku wengine wakitumia mashirika mengine ya ndege. Aidha, matumizi ya treni Saudi Arabia yameendelea kurahisisha ibada.

Mahujaji 96.85% hawakuwa na mahitaji maalum ya chakula, wakati 3.15% walihitaji lishe maalum kutokana na hali za kiafya kama kisukari, figo na shinikizo la damu. Hii inahitaji mfumo wa mapema wa taarifa za afya na mikataba ya huduma maalum.

Kwa upande wa afya, mahujaji wengi walikuwa salama, ingawa walitokea wagonjwa 9 waliolazwa hospitalini, 47 waliopata matibabu katika vituo vyetu vya Mina na Arafa, na mahujaji wawili walifariki. Tunawaombea rehema marehemu hao.

Mheshimiwa Waziri, Tathmini ya ibada za Hijja imeonesha kuwa, katika Twawaf na Sa'I Mahujaji 3,874 (96.85%) walitekeleza ibada wenyewe, huku 126 (3.15%) wakitumia vigari kutokana na uzee au changamoto za afya. Hii inaonesha umuhimu wa tathmini ya afya kabla ya safari na maandalizi ya huduma maalum.

Mahujaji waliopigiwa Jamarati waliongezeka kadiri siku zilivyopita :-

- Siku ya 10: 8.18%
- Siku ya 11: 9.6%
- Siku ya 12: 14.75%

Mwenendo huu unaashiria changamoto za uchovu, maradhi na uelewa mdogo wa taratibu za kisharia. Hivyo, Kamisheni inapendekeza mafunzo ya vitendo, maandalizi ya utimamu wa mwili na mpangilio wa mapema wa uwakilishi kwa wanaostahiki kusaidiwa.

Mahujaji na viongozi 3,626 (90%) walilipiwa kuchinja kupitia mfumo rasmi wa Nusuk, huku 414 (10%) wamebainisha kuwa watafunga. Kwa kweli suala la utekelezwaji wa wajibu huu wa kuchija au kwa kufunga kwa mahujaji hao 414 unatia shaka.

Mheshimiwa Waziri, Tathmini inaonesha kuwa zaidi ya nusu ya mahujaji (53.2%)

walionesha kuridhishwa kwao kikamilifu na huduma zilizotolewa, hususan mafunzo, afya, usafiri na uratibu wa viongozi. Changamoto zilizoorodheshwa na idadi kubwa ya mahujaji ni makazi Makka, Chakula Makka, huduma za vyoo Mina, Kuchanganyika na mataifa mengine Minna na kutopata taarifa muhimu kwa muda muwafaka kwa mahujaji na baadhi ya mashirika.

Gharama za Hijja kwa mwaka huu zilikuwa ni baina ya USD 5293 (ukitoa offer ya 5100) na USD 6754 kwa daraja "D" pakiwa na tofauti ya USD 1,461. Aidha, walikuwepo mahujaji 50 ambao walichukua huduma maalum za mahema ya "class A" kwa Minna na Arafa ambao walilazimika kuongeza gharama zake USD 5000 wakati mahema ya kawaida ni USD1032.

Mheshimiwa Waziri, Maandalizi ya Hijja ya mwaka 1448H/2027M yameshaanza tokea mwezi 12 DhulHijja na jana Juni 30,2026 kulikuw na warsha ya kimtandao kwa Ofisi zote za Hijja ulimwenguni. idadi ya mahujaji inatarajiwa kufikia 4,400, hivyo maandalizi ya mapema ni ya msingi sana ili kupata huduma nzuri.

Mheshimiwa Waziri, Mfuko wa Hijja Zanzibar unaendelea kukua ukiwa na wanachama 45, akiba ya zaidi ya TZS milioni 45.39 na USD 5,558, na tayari umewezesha mwanachama wa kwanza kuhiji kupitia mfumo wa akiba.

Katika eneo la Ziara za Kidini na Utalii wa Kiislamu, taarifa za misikiti mikongwe 51 na wasifu wa masheikh 7 mashuhuri zilikusanywa na kuhifadhiwa, hatua inayoweka msingi wa maendeleo ya Utalii wa Kiislamu Zanzibar.

Mheshimiwa Waziri,

Kwa niaba ya Kamisheni, napenda kutoa shukrani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Hijja na Umra Saudi Arabia, UTAHIZA, BAKWATA, mashirika ya Hijja na wadau wote.

Nimalizie kwa maneno ya Mtume (S.A.W): "Kila mmoja wenu ni mchungaji na ataulizwa kuhusu alichokichunga". Kwa pamoja, tuendelee kujenga mfumo wa Hijja ulio bora zaidi wenye uwazi uwajibikaji na huduma zinazokidhi matarajio ya mahujaji wetu na Taifa letu.

Mheshimiwa Waziri, Kwa heshima kubwa sasa namkaribisha Alhaj Prof. Issa Ziddy Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi ya Kamisheni azungumze chochote kisha kukukabidhi rasmi Ripoti ya Hijja ya mwaka 1447H/2026M na kukukaribisha utoe nasaha zako.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

Wassalamu Alaikum Warahmatullahi Wabarakatuh.

---

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ، قَالَ : سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ

«مَنْ حَجَّ لِلَّهِ فَلَمْ يَرْفُثْ وَلَمْ يَفْسُقْ، رَجَعَ كَيَوْمِ وَلَدَتْهُ أُمُّهُ»

{ مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ }

Kutoka kwa Abu Hurairah (r.a.) amesema: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) akisema: "Mwenye kuhiji kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kisha asiseme maneno machafu wala maasi, atarudi akiwa msafi wa dhambi kama siku aliyozaliwa na mama yake."

(Imepokewa na Al-Bukhari na Muslim).